**Learning by Ear**

**People Who Make a Difference**

**Children-Parliament (Nigeria)**

Author: Hakeem Jimo, Nigeria

Editor: Stefanie Duckstein

Translator: Anthony Dunham (marked in red: corrected English)

Sound clips in DALET: Learning by Ear: **LbEKidParliamentNigeria**

CHARACTERS:

Announcer:

- Young (male) voice

Sound clips: (1 woman und 2 young women)

- Head teacher (around 35)
- School friend (around 16)
- Esther (16)

**Introduction (Announcer):**

Karibu msikilizaji wa Noa Bongo Jenga Maisha Yako, ni matumaini yangu kuwa hujambo. Katika makala haya ya “watu wanaoleta mabadiliko” utakutana na baadhi ya mashujaa wa kawaida katika maisha ya kila siku kutoka barani Afrika. Watu hao ni mashujaa, wakweli na wamejitolea kwa moyo wao wote.

Hawavunjwi moyo na matatizo ya kila siku. Wana ndoto ya maisha ya usoni.

Leo hii utakutana na Esther, msichana mdogo mwanasiasa kutoka Nigeria.

--------------------------------

**TEXT:**

1. **ATMO STREET** (Bring up at end of Intro, let run for 5 seconds and fade under OTON)**:**

2. **OTON Esther1:**

"Nimekulia hapa. Na hapa ndio kwetu. Nimeishi hapa maisha yangu yote. Hapa ndipo nilipozaliwa, nimezoa mazingira ya hapa. Ninaweza kwenda kokote, ninajua kila mahala. Najua kona zote za mahala hapa."

3. **ATMO STREET** (Up again for 5 seconds then down again)**:**

4. **NARRATOR:**

Esther Afolayan ana miaka 16. Yeye ni rais wa Senate katika bunge la watoto nchini Nigeria. Lakini imemchukua muda mrefu kufikia kwenye madaraka hayo. Kutoka kuzaliwa kwake, Esther ameishi kwenye mji mkubwa wa Lagos. Mpaka sasa anaishi kwenye nyumba ile ile aliyozaliwa mjini humo ijapokuwa wazazi wake pamoja na ndugu zake wamehamia mahala pengine mjini humo. Baba yake anafanya biashara ya kuuza vifaa vya ujenzi na mama yake ni mwalimu wa shule ya msingi. Esther anaishi hapo kwa sababu anataka kumaliza masomo yake.

**5. OTON Esther3:**

"Hii ni nyumba yetu na nyumba hii ni maisha yangu yote. Nimekulia hapa, nimeishi hapa tangu nizaliwe miaka 16 iliyopita. Nasoma hapa. Na kila kitu ninachofanya kiko katika maeneo haya. Tuliishi hapa na familia yangu yote, yaani tulikuwa wapangaji, labda niseme wenye nyumba hii ni marafiki wakubwa wa familia yangu. Bibi yangu, Baba, Denrele, Jumoke na shangazi Dupe pamoja na ndugu wengi tu kutoka kwenye familia yetu walikaa hapa zamani. Kwa hivyo nyumba hii sisi huwa tunaifanyia marekebisho tu."

**6. ATMO House renovation** (fade in shortly before the end of OTON 2 and establish for 3 seconds, fade under)

**7. NARRATOR:**

Kila mara kuna kitu kinachohitaji kurekebishwa. Si ndani ya nyumba peke yake bali hata nje kwenye barabara, kwani serikali ina mambo mengi ya kufanya anasema Esther.

**8. OTON Esther2:**

"Gavana wetu anafanya kazi nzuri sana. Hii barabara ilikuwa mbaya mno. Uuhh! Kila kitu hapa kilikuwa kimeharibika. Lakini sasa kila kitu kiko sawa. Unaweza kutembea unavyotaka. Si vibaya."

**9. NARRATOR:**

Haikuwa hivyo. Serikali ya majimbo au serikali kuu zilikuwa hazishungulikii mahitaji ya wananchi. Nchini Nigeria watu wamezowea mambo kivingine, ni sawa na kusema kuwa wanasiasa na matajiri hawajali mahitaji ya watu masikini, hawajali hata watoto.

**10. OTON Esther5:**

“Kama wakristo tunawajibika kuwajali wenzetu. Hata kama sio wakristo lakini kama binadamu tuna hisia. Kuna watu ambao wanafaidi mambo ambayo hata hawakuyafanyia kazi. Au kuna watu ambao wanafurahia vitu lakini hawawafikirii wale ambao hawana vitu hivyo.”

**11. NARRATOR:**

Kila mara msichana mdogo Esther anapoyafikiria haya, anafumba na kufumbua macho yake. Je ni wakati gani alipoamua kwamba ni lazima achukue hatua itakayoleta mabadiliko?

**12. OTON Esther7:**

“Ninakumbuka niliangalia kipindi kimoja. Niliona hali mbaya sana, ilikuwa kama vile... .Mungu wangu!...kweli kuna watu wanaoteseka namna ile. Sikujua yule mwanamke alikuwa amemfanya nini mtoto wake, lakini nilisikia alikuwa amemfanyia mtoto wake mambo mabaya ya kutisha. Mimi nilikuwa najiuliza sisi ni watoto, si nilidhani tunapaswa kutunzwa? Nilidhani tunapaswa kuangaliwa vyema kama mayai? Nilishangaa upendo na matunzo vilikwenda wapi wakati watoto wale walipokuwa wanataabika namna ile. Niliwaza kuwa watoto wale walihitaji sauti ya kuwatetea kwa sababu wao hawakuwa na sauti hiyo”

**13. NARRATOR:**

Ni shuleni alikopata fursa ya kuandika insha kuhusu haki za watoto.

**14. OTON Esther4:**

“Nadhani kichwa cha insha hiyo kilikuwa, 'Yatima na watoto walio katika hatari

ya kuathirika - ni jukumu la nani? La serikali au la jamii ?" yaani nani hasa anapaswa kuwa na jukumu la kuwalea watoto yatima na watoto wengine walio katika hatari ya kuathirika na mikasa mbalimbali? Je jukumu ni la serikali peke yake au jamii nzima inaweza kushiriki kuwasaidia watoto hawa kuishi?."

**15. ATMO SCHOOL PLAYGROUND** (Establish for 7 seconds, then fade down under NARRATOR then up again for 5 seconds)**:**

**16. NARRATOR:**

Esther, anatambuliwa sio tu na rafiki zake bali hata na mwalimu wake mkuu na wengine wote wanaomtambua kwa sababu kila anachokifanya, anakifanya vizuri.

**17. OTON Friend1:**

"Jina la shule yetu limefika mbali kwa sababu kuwa na rais wa Senate wa bunge la watoto ambae anatoka kwenye shule yenu ni sifa kubwa! Wacha niseme huo ni mfano wa kuigwa. Ndio! Kila mmoja wetu anamuona kuwa yeye anaweza kutoa wazo kwa sababu yeye ni msemaji mzuri. Anapenda kuwa na watu. Yale aliyoyafanya na anayoyafanya sasa, hakika ni changamoto kubwa kwa watu wengine. Ni mfano mwema kwa sababu mtu anahitajika kujaribu kufanya kitu kitakacholeta mabadiliko ."

**18. ATMO SCHOOL PLAYGROUND** (fade up again for 3 seconds)**:**

**19. OTON HEADTEACHER2:**

"Natumai kwa uwezo wa mungu Esther atafika mbali sana. Amekuwa mfano mwema kwa wanafunzi wenzake. Niliandamana naye mara moja wakati

alipokwenda kuwasilisha mswaada wake. Alifanya vizuri sana, sikuwa na la kuongeza. Wanafunzi wenzake wa MGHS wanampenda sana. Wanamuona kama mtu anayeweza kuwawakilisha."

**20. NARRATOR:**

Ruth Olusheye Awobiyi ni mwalimu mkuu wa shule ya upili ya wasichana ya Methodist iliyopo katika kitongoji cha Yaba, katika jiji la Lagos. Mwaka jana alitunukiwa tuzo ya mwalimu mkuu bora kati ya shule zote 70 za wa misionari nchini Nigeria. Alipata mchango mkubwa kutoka kwa Esther, kwanza alipokuwa naibu msemaji wa bunge la watoto katika mji wa Lagos na sasa yeye ndiye rais wa Senati ya bunge la watoto nchini Nigeria.

**21. OTON Esther6:**

"Nia hasa ya kuanzishwa kwa bunge la watoto ni kwa sababu ya kutetea haki za watoto. Kuna watoto wengi ambao hawakubahatika, lakini hata wale waliobahatika wote wamo katika hatari ya kuathirika. Kwa hivyo bunge la watoto liliundwa ili watoto hao wapate fursa ya kusema wanachotaka kifanyike na kitekelezwe. Kwa hivyo nikaona kuwa hapa ni sehemu inayostahili kwa watoto kutimiza malengo hayo."

**22. NARRATOR:**

Esther husafiri takriban kilomita 1000 katika mji mkuu wa Abuja kila baada ya miezi michache wakati wa likizo, au siku za wikiendi ikiwa ni baadhi ya majukumu aliyo nayo kama rais wa Seneti katika bunge la watoto nchini Nigeria. Safari yake hiyo humwezesha kukutana na watoto wa majimbo yote nchini. Zaidi ya wajumbe 70 hukutana kujadili shida mbalimbali zinazowakabili watoto katika nchi yenye watu milioni 140. Vifo vingi vya watoto na watoto wanaoishi

kwenye mazingira magumu nchini Nigeria, ni hali inayomsikitisha sana Esther.

**23. OTON Esther8:**

"Tatizo kubwa nililoligundua ni kwamba hata watoto wenyewe hawajui haki zao. Katika swala la unyanyasaji wa watoto sitoi dhamana kwa watoto wanaochuuza vitu barabarani. Badala yake huwa nawauliza kwa nini hawaendi shule?" wananiangalia tu kana kwamba wanajiuliza 'na huyu nae anasema nini?' Nafahamu kwamba ni lazima niulize hivyo kwa sababu iwapo nitanunua vitu kutoka kwao ni sawa na kuwa ninawaunga mkono kuendelea kuchuuza vitu barabarani. Naamini kwamba tukiendelea kuwauliza kwa nini hawaendi shule basi hii itasaidia japo mmoja wao atamwambia mzazi wake siku moja kuwa na yeye anataka kwenda shule. Ninawasiliana na rafiki zangu na wanafunzi wenzangu darasani. Shuleni tuna fursa ya kuandika makala kwenye gazeti la shule."

**24. NARRATOR:**

Je, Esther ana malengo ya kujiendeleza kutoka kwenye bunge la watoto hadi kwenye bunge la taifa?

**25. OTON Esther9:**

"Ninataka kusomea sayansi ya Kompyuta, napenda Kompyuta. Kuna mambo mengi ningependa kufanya. Ningependa kusomea sheria pia lakini napenda zaidi Kompyuta. Ninampongeza sana mtu aliyevumbua Kompyuta kwa sababu inarahisisha kazi. Ukitaka kufanya kazi fulani, Kompyuta itafanya kazi hiyo kwa sekunde mbili au tatu. Ninataka kujua mengi kuhusu kompyuta. Mambo ambayo siyo ya jumla, ambayo kila mtu anajua kwamba kompyuta inaweza

kufanya hili ama lile.  Kwa habari za kina. Hicho ndicho ninachokifanyia utafiti."

**OUTRO (Announcer):**

Esther anapendelea kuchunguza kiini cha jambo. Alimweleza mwandishi wa hadithi hii Hakeem Jimo kabla hajaingia katika mkahawa wa Intaneti ulio karibu. Na hiyo ndio hadithi kumuhusu Esther. Iwapo ungetaka kusoma zaidi au kusikiliza tena kipindi hiki, tembelea mtandao wetu kwenye anuani ifuatayo: www.dw-world.de/lbe.

Asante kwa kusikiliza na ni matumaini yangu kuwa utaungana nasi tena wakati ujao katika hadithi nyingine mpya kwenye makala ya Noa Bongo jenga Maisha yako kuhusu watu wanaoleta Mabadiliko.  Hadi mara nyingine, Kwaheri!

END